



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BARIADI

Telegrams "MAJI Tel No: 028-2700204

S.L.P 64, Bariadi

Fax: 028-2700204, Barua pepe: md@baruwasa.go.tz



**Kumb:Na.BRD/WSSA/MoW/014/462**

14/03/2022.

Katibu Mkuu,  
Wizara ya Maji,  
S.L.P 456,  
**DODOMA.**

**YAH: MAOMBI YA FEDHA KIASI CHA SHILINGI 36,750,000.00 KWA AJILI YA KAZI ZA NYONGEZA KATIKA MRADI WA DHARURA YA KUKABILIANA NA UVIKO-19.**

Tafadhali husika na mada tajwa hapo juu.


Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Bariadi (**BARUWASA**) inaleta maombi ya kulipwa kwa fedha kiasi cha shilingi **36,750,000.00/=** (*Milioni thelathini na sita, laki saba na hamsini tu*) kwa ajili ya kazi ya fundi mjenzi (*Local fundi*) anaefanya kazi za kupeleka nishati ya umeme kwenye vyanzo vya Maji vilivyopo Izunya na Mahina kama malipo ya nyongeza.

Kazi hii ilisaulika wakati wa kuandaa gharama halisi za Mradi wa kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19 unaoendelea. Hadi sasa Utekelezaji wa Kazi Umefikia asilimia 50. Mkatiba wa kazi hii umeambatishwa kwa rejea.

S/N	Jina la Fundi Mjenzi ( <i>Local Fundi</i> )	Kazi anayofanya.	Fedha ambayo haijalipwa.
1	M/S Pentagon Electrical Services. ( <i>Local fundi</i> )	Kazi ya fundi wa kufikisha nishati ya umeme kwenye vyanzo viwili vya Izunya na Mahina.	36,750,000.00/=
<b>Jumla</b>			<b>36,750,000.00/=</b>

Wako katika utumishi wa umma.

Eng. Musalika Masatu  
**MKURUGENZI MTENDAJI.**






**WIZARA YA MAJI**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BARIADI**

Telegrams "MAJI Tel No: 028-2700204 S.L.P 64, Bariadi

Fax: 028-2700204, Barua pepe: mdbaruwasa@yahoo.com



**MKATABA MDOGO WA AJIRA ZA MAFUNDI**

**KATI YA**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA BARUWASA S.L.P 64, BARIADI, SIMIYU**

**NA**

**PENTAGON ELECTRICAL SERVICES S.L.P 702, SHINYANGA**

**KWA**

**KAZI YA KUPELEKA UMEME KWENYE VYANZO VYA MAJI VYA SANUNGU  
MAHINA, IZUNYA NA NYAUMATA**

**MKATABA NA.BRD/UWASA/POWER/ 2021-2022/W/02**

**Novemba, 2021**



**FOMU F2: MKATABA MDOGO WA AJIRA ZA MAFUNDI**

**KAZI YA KUPELEKA UMEME KWENYE VYANZO VYA MAJI VYA  
SANUNGU MAHINA, IZUNYA NA NYAUMATA**

---

**MKATABA HUU** unafanyika leo tarehe 25 mwezi Novemba,  
2021....

**BAINA YA**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BARIADI  
(BARUWASA) S.L.P 64** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama  
"Mwajiri au BARUWASA") kwa upande mmoja;

**NA**

**Pentagoni Electrical Servises S.L.P 702 SHINYANGA** (ambaye katika  
Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiriwa au Fundi") kwa upande  
mwingine.

**KWAMBA** kwa pamoja Mwajiri na Mwajiri watajulikana kama pande mbili za  
Mkataba.

**AMBAPO:**

- a) Mwajiri ni Mamlaka ya maji wenye jukumu la kutekeleza ujenzi wa  
miradi ya maji mjini na kusimamia utoaji wa huduma ya maji na  
usafi wa mazingira mjini.
- b) Mwajiriwa ni mtu binafsi anayefanya shughuli zake binafsi za ujenzi  
**Shinyanga;**
- c) Mwajiri anakusudia kumwajiri Mwajiriwa kwa kipindi cha muda  
mfupi wa miezi miwili;
- d) Mwajiriwa anakubali matakwa ya Mwajiri na anakubali kwa hiari  
yake mwenyewe kuajiriwa kwa muda mfupi kama fundi wa kupeleka  
nishati ya umeme kwenye vyanzo vya maji vya Mahina na Nyaumata.

**MKATABA HUU UNASHUHUDI** kwa pande zote mbili kukubaliana kama  
ifuatavyo:



### **1. MADHUMUNI YA MKATABA**

Mkataba huu ni kwa ajili ya Kupeleka nishati ya umeme kwenye vyanzo vya maji vya Sanungu Mahina ,Izunya na Nyaumata. Mwajiriwa atapaswa kufanya kazi zifuatazo:

- Kujenga njia kuu ya umeme yenye msongo wa 33Kv kutoka kwenye nguzo ya kuchukulia umeme (taping poles) mpaka kwenye transfoma
- Kujenga vituo vya transfoma kwenye vyanzo vya Mahina na Nyaumata
- Kujenga 'service line' kutoka kwenye transfoma kwenda kwenye vyanzo vya maji vya Sanungu Mahina, Izunya na Nyaumata .

### **2. MUDA WA UTEKELEZAJI WA KAZI**

Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 60, ambapo itaanza tarehe 25/11/2021 na itakamilika tarehe 25/1/2021

### **3. MALIPO YA UTEKELEZAJI WA KAZI**

- a) Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha Tshs **36,750,000/=**kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu;
- b) Malipo ya Mwajiriwa yatakuwa ni fedha za kitanzania tu (*Tanzanian Shillings*);
- c) Malipo hayo yatalipwa kwa hundi ambayo italipwa benki;
- d) Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa kwa awamu mbili (2) kama ifuatavyo:
  - i. Malipo ya awamu ya kwanza ya Tsh **23,426,000** yatalipwa mara baada ya kukamilisha kazi ya kupeleka nishati ya umeme kwenye vyanzo vya maji Izunya na Nyaumata .
- e) Malipo ya yanayobaki ya Tsh **13,324,000/=** yatalipwa mara baada ya kukamilisha kazi ya kupeleka nishati ya umeme kwenye vyanzo vya maji vya Sanungu Mahina ujenzi wa mradi.
- f) Kabla ya malipo ya mwisho kufanyika,Mwajiriwa anapaswa kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika na kufanya marejesho ya vifaa vyote vya kazi na fedha za mradi kama zitakuwepo.

### **4. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRI**

Mwajiri ambaye atawakilishwa na Msimamizi wa Kazi, atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

- i. Kutoa vifaa vyote kwa ajili ya uchimbaji wa kazi hii;
- ii. Kusimamia na kuthibitisha ubora wa kazi inayofanywa na fundi;
- iii. Kuwasiliana na uongozi wa eneo husika namna ya kuwashirikisha wananchi/Jumuiya ya Watumia Maji katika shughuli za ujenzi wa Mradi;



- iv. Endapo kazi itakayofanywa na Mwajiriwa haitafikia viwango vya ubora unaotakiwa, Mwajiri atachukuwa hatua stahiki dhidi ya Mwajiriwa huyo; na Msimamizi wa Mradi ata mtaarifu fundi wa kazi hii kwamba ameshindwa kutimiza masharti ya makubaliano
- v. Kuhakikisha kuwa endapo Mwajiriwa atafanya kazi isiyokidhi viwango au isiyoridhisha, Mwajiriwa huyo anarekebisha au kurudiwa upya kazi hiyo kwa gharama zake mwenyewe.

#### **5. HAKI NA WAJIBU WA MWAJIRIWA**

Mwajiriwa ambaye ni fundi atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:

- a) Kuhakikisha kuwa anatekeleza ujenzi wa kazi zote kama zilivyoelekezwa kwenye sehemu ya 1 (Madhumuni ya Mkataba) kulingana na ramani na vipimo viliyotolewa na Mwajiri;
- b) Kuhakikisha kuwa anawajibika kufanya kila jambo ambalo kwa ujumla wake litaleta mafanikio kwenye mradi atakaoujenga;
- c) Atatekeleza majukumu yake kwa uaminifu, uadilifu, umakini na weledi mkubwa na endapo atatekeleza kinyume na matakwa haya, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake;
- d) Atawajibika kwa Msimamizi wa Mradi (*Project Manager*) kwa utendaji wake wa kila siku na atatekeleza maelekezo anayopewa na kiongozi huyo;
- e) Atawajibika kuhudhuria mikutano ya tathmini ya mradi pamoja na watendaji wengine wa timu yake kila itakapopangwa;
- f) Atawajibika kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mradi kila zitakapohitajika;
- g) Kuhakikisha malipo ya vibarua na mafundi walioajiriwa kwa mikataba midogo yanafanyika kwa wakati; na
- h) Kufanya usafi eneo la ujenzi wa mradi na kuondoa mabaki yote ya vifaa vya ujenzi na kuviweka katika eneo litakaloelekezwa na Msimamizi wa Mradi.

#### **6. UTOAJI WA MIKATABA MIDOGO**

Mwajiriwa anaweza kuingia Mikataba midogo kiasi kadhaa ya utekelezaji wa kazi na vibarua (*casual labourers*) watakaokuwa chini ya usimamizi wake.

#### **7. UCHELEWESHAJI WA UTEKELEZAJI WA MRADI**

Endapo kazi haitakamilika katika muda uliopangwa, Mwajiriwa atalipa faini ya asilimia 5 ya malipo ya kazi yote kwa kila siku ya ucheleweshwaji isipokuwa kukiwa na sababu ya msingi ya ucheleweshwaji wa kazi ulioidhinishwa kwa maandishi na Msimamizi wa Mradi.



## **8. DHAMANA YA UHARIBIFU**

Mwajiriwa atawajibikakulipa gharama za uharibifu au madhara yoyote yatakayosababishwa na wafanyakazi wake au vifaa vyake wakati wa utekelezaji wa mradi; na

Gharama hizo au madhara hayo yatabainishwa na Msimamizi wa Mradi kwa maandishi.

## **9. SHERIA ITAKAYOTUMIKA**

Mkataba huu utaongozwa na kusimamiwa na Sheria za Tanzania.

## **10. USULUHISHI WA MGOGORO**

Endapo kutatokea mgogoro wa aina yoyote baina ya Mwajiri na Mwajiriwa kuhusu utekelezaji wa mradi huu:

- a) Pande zote mbili zitatatua mgogoro huo kwa njia ya amani ya mazungumzo ambapo makubaliano ya pande hizi mbili yatapelekea Mkataba huu kufanyiwa marekebisho; na
- b) Endapo mgogoro huo utashindikana kutatatuliwa kwa njia ya amani ya mazungumzo, pande zote mbili zinaweza kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

## **11. KUSITISHA MKATABA**

Mkataba huu unaweza kusitishwa endapo upande mmoja au pande zote mbili za Mkataba zitashindwa kutekeleza wajibu wake au masharti ya Mkataba huu.

## **12. MAREKEBISHO YA MKATABA HUU**

Kwamba Mwajiri na Mwajiriwa wanaweza kubadilisha baadhi ya masharti ya Mkataba huu kwa makubaliano ya pamoja kwa njia ya maandishi.

## **13. MASHARTI YA NYONGEZA**

Masharti mahsusi ya nyongeza kuhusiana nautekelezaji wamradi huu ni pamoja na:

- a) Mvua kuzidi kunyesha na kusababisha kushindwa kuingia eneo la kazi
- b) Kuchelewesha vitendea kazi (construction materials)
- c) Kuchelewa kwa Malipo




KWA USHUHUDA HUU, pande zote mbili zinaweka sahihi zao katika Mkataba huu siku na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini:


**MWAJIRI (BARUWASA)**

**Shahidi:**

Jina: Modira Maaty


Jina: Chadwick W. Munde

Sahihi: 

Sahihi: 

Cheo: 

Cheo: Technical Manager

Tarehe: 

Tarehe: 25/11/2021


**MWAJIRIWA (FUNDI)**

**Shahidi:**

Jina: Nani SINDO NDESIRWA

Jina: Charles Eustid Muchunza

Sahihi: 

Sahihi: 

Cheo: M.B.

Cheo: Technical Manager

Tarehe: 25/11/2021

Tarehe: 25/11/2021

FOMU F3: MAHITAJI YA KAZI

JINA LA MRADI: MRADI WA KUPELEKA UMEME KWENYE VYANZO

NA	MAELEZO YA KAZI (DESCRIPTION)	KIPIMO (UNIT)	KIASI (QUANTITY)	BEI (COST)	GHARAMA (AMOUNT)
1	Kujenga njia kuu ya umeme yenye msongo wa 33Kv kutoka kwenye nguzo ya kuchukulia umeme (taping poles) mpaka kwenye transfoma	km	3	5,606,500	11,213,000/=
2	Kujenga vituo vya transfoma kwenye vyanzo vya Mahina na Nyaumata	nr	2	6,756,000	13,512,000/=
3	Kujenga 'service line' kutoka kwenye transfoma kwenda kwenye vyanzo vya maji vya Sanungu Mahina, Izunya na Nyaumata	nr	2	6,12,500	12,025,500/=
<b>JUMLA KUU</b>					<b>36,750,000/=</b>